

## **Utangulizi**

Kamusi ni kitabu chenye vipengele vya kileksia vinavyopangwa kwa utaratibu fulani au muundo, kikiwa na taarifa muhimu kuhusu vipashio hivyo (Elkateb, 2014). Miongoni mwa vigezo vinavyotumiwa kuainisha kamusi ni lugha. Vigezo vingine ni ukubwa, walengwa na maudhui. Taarifa inayotolewa inaweza kuwa katika lugha moja na kuunda kamusi Wahidiya au katika lugha mbili (Kamusi Thaniya) au lugha zaidi ya mbili na kuunda Kamusi Mahuluti. Kamusi thaniya na mahuluti hutumiwa katika mchakato wa tafsiri na pia hujulikana kama kamusi ya wingilugha. Jamii nyingi ulimwenguni huwa jamii lugha ulumbi ambapo lugha zaidi ya mbili huzungumzwa. Sura hii inajadili tafsiri tenge kwenye kamusi thaniya ya Kiingereza-Kiswahili (TUKI, Toleo la Tatu).